

**JIMBO KATOLIKI IRINGA**  
**TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI TOSAMAGANGA (TIHAS)**



S.L.P 50 TOSAMAGANGA  
IRINGA

SIMU: 0769 432 532 (MKUU WA TAASISI)/ 0762 482 704 (MHASIBU)

BARUA PEPE: [tosamagangainstitute@gmail.com](mailto:tosamagangainstitute@gmail.com)

TOVUTI: [www.tihac.ac.tz](http://www.tihac.ac.tz)

**UTANGULIZI**

Tunayofuraha kukuaribisha hatika Tasisi yetu ya Afya na Sayansi Shirikishi Tosamaganga. Taasisi inakuarifu tarehe ya kufungua mwaka mpya wa masomo wa 2022/2023 kwa mkupuo wa mwezi wa tisa itakuwa ni tarehe **15/10/2022**.

**MUHIMU**

Taasisi pia imefikia maridhiano na serikali ya wanafunzi kusitisha huduma ya chakula kilichokuwa kinatolewa na Taasisi, hivyo wanachuo wetu watajitegemea kwa kununua chakula kwa bei nafuu katika kantini inayopatikana ndani ya Taasisi.

**GHARAMA ZA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA (ORDINARY  
DIPLOMA IN NURSING AND MIDWIFERY) MWAKA WA PILI**

Na	AWAMU	ADA	MALAZI (Hostel)
1	Awamu ya kwanza (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza)	500,000	BURE
2	Awamu ya pili (mwezi Februari)	500,000	BURE
3	Awamu ya tatu (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)	500,000	BURE
4	Awamu ya nne (Mwezi Julai)	500,000	BURE
	<b>JUMLA</b>	<b>2,000,000/=</b>	<b>BURE</b>

**NB:**

1. Gharama za Ada, Chakula na Malazi iliyoainishwa kwenye jedwali ilipwe kwenye Kumbukumbu namba ya malipo (**Control Number**) ya mwanachuo kupitia Benki ya CRDB.
2. Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya uchumi wa Taasisi, Jimbo na Nchi.
3. Ada unaweza kulipa yote au kwa awamu nne kama ilivyoainisha kwenye jedwali
4. Mwanafunzi asipotimiza kulipa ada kwa awamu husika hatapokelewa au atarudishwa nyumbani na akikaa nyumbani kwa muda wa siku 21 na zaidi atapaswa kurudia mwaka.
5. Wale tu ambao wamelipa nusu ya ada ya muhula ndio watakasajiliwa kwenye muhula husika.
6. Ada ikishalipwa hairudishwi.

**ADA YA MAZOEZI KWA VITENDO**

1. Wanafunzi watafanya mazoezi kwa vitendo katika katika jamii (Community field) kwa mwaka wa pili. Gharama za mazoezi kwa vitendo ni **Tsh. 150,000/=** mwanafunzi aje nayo mkononi wakati wa kuripoti muhula wa pili.

**MICHANGO MINGINE**

1. Gharama ya mitihani ya taifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni **Tshs.150, 000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
2. Ada ya Udhhibiti Ubora (Quality Assurance Fee) **Tshs.15, 000/=** Kwa ajili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (**NACTVET**), UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
3. Matibabu **Tshs.52,400/=** kwa asiye na bima na kwa mwenye bima afike na bima yake (UJE NA FEDHA MKONONI)
4. Mfuko wa serikali ya wanachuo ni **Tsh 10,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
5. Gharama za usajili kwenye Baraza la Uuuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) **Tshs 50,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti kama hukulipa mwaka kwani huwa inalipwa mara moja tu kwa miaka yote mitatu ya masomo.
6. Gharama za marudio ya mtihani (supplementary exam) ni **Tsh. 30,000/=** kwa somo (kwa atakae shindwa fikia wastani) na maombi ya mtihani maalumu (Special sit exam) ni **Tsh. 50,000** kwa kila somo ( kwa sababu maalum)

Tunakutakia maandalizi mema na KARIBU.

ASANTE

ERICK L. MSEMWA  
MKUU WA TAASISI



TIHAS